


Samaki mkarimu

Kholeka Mabeta
Kiswahili





Hapo zamani za kale palikuwa na mtu aliyeitwa Mpunzi.

Alikuwa na mke na mtoto mmoja aliyeitwa Nosisa.

Mpunzi alitaka mtoto mvulana, lakini yeye na mkewe hawangeweza kupata watoto wengine.

Mpunzi alimlaumu mkewe kwa kutompa mtoto wa kiume.

Siku moja, Mpunzi alimgonga mkewe kwa fimbo.

Mkewe alitorokea nyumbani kwa familia yake.
Alihuzunika kwani Mpunzi hakumruhusu aende na
Nosisa.

Mpunzi alimdhulumu bintiye namna alivyomdhulumu
mkewe.

Nosisa aliishi maisha ya huzuni sana.





Mpunzi alioa mke mwingine. Alitumaini kwamba mke huyu mpya angemzalia mtoto mvulana.

Maisha ya Nosisa sasa yalikuwa magumu zaidi wakati babake alioa tena.

Mpunzi alimtetesha wakati wote na kumlazimisha kumtumikia mke wake mpya.

Nosisa alifanya kazi kama mtumwa.


Mpunzi aliona fahari sana kutokana na mifugo wake.

Alizoea kukaa nje ya boma lake na kuangalia mifugo wake wakila nyasi uwanjani. Alihisi kuwa ametosheka sana na mali yake.

Wengi wa wafanyi kazi wa Mpunzi walifagia boma lake, na kuwaangalia mbuzi, farasi, mifugo na kondoo wake.

Waliwakama ng'ombe maziwa ambayo Mpunzi aliwauzia wanakijiji wengine.





Mpunzi alimpenda mke wake mpya sana na kumchukulia kama malikia.

Alikaa chumbani wakati wote huku akiwaamrisha Nosisa na wafanyi kazi.

Nosisa alirauka mapema kila siku kumtayarishia chai mamake wa kambo.


Alimfagilia chumba chake na kumpikia, lakini mamake wa kambo alinung'unika kuwa chakula chake kilikuwa baridi, kuwa chai yake ilikuwa hafifu, na kwamba chumba chake hakikuwa kisafi.


Siku moja Mpunzi alikasirika, akamkaripia na kumgonga Nosisa kwa kijiti.

Nosisa alikimbilia mtoni alikokaa na kulia alasiri nzima. Ghafla, alisikia sauti ikitokea mtoni.

Aliangalia juu na kumwona samaki mkubwa aliyetoa sauti.

Nosisa alishtuka karibu kutoroka, lakini samaki alimkatiza, “Tafadhali binti yangu usitoroke, mimi ni mamako. Nimejibadilisha kuwa samaki ili babako asigundue kwamba ni mimi.”





“Ni nini ndiyo shida?” samaki aliuliza. Nosisa alimwambia samaki kuhusu maisha yake ya huzuni.

“Usiwe na wasiwasi msichana wangu. Nitakuletea chakula kila siku,” samaki alisema.

Samaki alimpa Nosisa mboga mbichi. Alikuwa na sherehe. Alipoangalia juu, samaki alikuwa ametoeka.


Siku hiyo Nosisa alienda nyumbani akitabasamu. Hataenda kulala tena bila chakula kama kawaida.

Nosisa alienda mtoni kila siku.

Asubuhi aliamka na kufanya kazi zote za nyumbani kama kawaida. Adhuhuri, alienda mtoni.

Aliitana kila wakati, na kila wakati samaki alitokea akiwa na chakula kitamu. Nosisa alifurahi zaidi na zaidi.

Angezungumza chochote na samaki. Alianza kupata afya yake. Ngozi yake ilianza kuangaza naye akawa mtoto mwenye furaha.





Nosisa alimtembelea samaki kila siku mpaka mamake wa kambo akawa anatilia shaka.

“Kuna jambo linatendeka kule mtoni, na lazima nigundue ni nini,” mama wa kambo aliwaza.

Alasiri moja alimfuata Nosisa mtoni. Alimwona Nosisa akimzungumzia samaki na kupokea chakula kitamu. Siri ya Nosisa ilikuwa nje.


“Lazima nifanye jambo kumhusu huyu samaki,” alisema mama wa kambo.

Jioni, Mpunzi alirejea nyumbani na kumpata mkewe mpya akilia ndani ya chumba chake.

“Nini kibaya mke wangu mrembo?” Mpunzi aliuliza.

“Mganga wa kienyeji aliniambia kwamba njia pekee ya kukuzalia mtoto mvulana ni kwa kumla samaki mkubwa anayeishi kwenye mto ulio karibu hapa,” alisema. “Utanishikia yule samaki usiku wa leo?” mwanamke alimsihi.

“Nitakufanyia lolote bibi yangu mrembo,” Mpunzi akasema.





Mpunzi alianza safari ya kwenda mtoni kabla giza kuingia.

Aliwachukuwa wafanyi kazi wake wamsaidie kumpata samaki aliye mkubwa zaidi katika mto ule.

Mpunzi alimpata samaki mkubwa zaidi. Alipofika nyumbani, kulikuwa na moto mkubwa tayari kumpika samaki.


“Nitatarisha kitoweo kizuri kwetu,” mwanamke akamwelezea Mpunzi aliyefurahia sana.


Usiku ule Mpunzi na mkewe walienda kitandani kulala baada ya chakula kitamu.

Waliacha mifupa mezani ili Nosisa asafishe asubuhi yake.

Wakati Nosisa alipowaletea kahawa chumbani, walikuwa bado wanalala.

“Hili ni jambo geni,” Nosisa alifikiria. “Babangu huamka mapema mno kwenda mashambani. Nastaajabu kwa nini yeye bado analala.”





“Haidhuru, naweza kukimbia mtoni kwa kiamsha kinywa kizuri,” alifikiria.

Nosisa alikimbia kwenda mtoni. Alipofika kule, alimwita samaki tena na tena. Samaki hakuwahi kuja.

Nosisa alianza kulia. Hakujuu kilichometendeka samaki.

Alipokuwa akilia, ndege alikuja na kukaa kando yake na kumwambia kilichotendeka.


Alilia kwa nguvu akidhani kwamba mamake alikuwa ameshikwa na kuliwa.

Ndege alimwambia aiokote mifupa kutoka mezani na kuirusha ndani ya mto.

Angefanya hivyo, samaki angefufuka.

Alimwambia pia awaache babake na mamake wa kambo walale hadi aduhuri.

Nosisa alifanya alivyoambiwa. Aliichukuwa mifupa, akiweka mfukoni kisha kuirusha mtoni.





Nosisa alikimbaia kurudi nyumbani na kabla aduhuri kufika, aliwaamsha babake na mamake wa kambo.

Hakuwatambua. Walizeeka na kudhoofika.
Hawangemkaripia wala kumpiga.
Walichoka wasiweze kuungalia mji wao.

Kwa hivyo, Nosisa alichukuwa mji wa babake pamoja na mali yake. Aliwaita wafanyi kazi wote na kuwaambia kilichotokea.

Walisherehekea na kuwa na amani katika mji huo kutoka siku hiyo.

Samaki mkarimu

Writer: Kholeka Mabeta


Illustration: Wiehan de Jager

Translated By: Brigid Simiyu

Language: Kiswahili



© African Storybook Initiative



This work is licensed under a Creative Commons Attribution
(CC-BY) Version 3.0 Unported Licence

Disclaimer: You are free to download, copy, translate or adapt this
story and use the illustrations as long as you attribute or credit the
original author/s and illustrator/s.

Saide 
South African Institute
for Distance Education
www.africanstorybook.org
A Saide Initiative